

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu: 255-22-2114512, 2116898  
E-mail: press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)  
Faksi: 255-22-2113425*



*OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA BARACK OBAMA,  
11400 DAR ES SALAAM.*

*Tanzania.*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli amefanya uteuzi wa mabalozi watatu katika Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa.

Rais Magufuli pia amefanya uteuzi wa makamishna wanne wa Jeshi la Polisi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Taarifa ya Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Ombeni Sefue, imewataja mabalozi walioteuliwa kuwa ni **Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro, Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe** na **Dkt. Ramadhan Dau.**

Vituo vya uwakilishi kwa mabalozi hawa vitajulikana baada ya taratibu husika za kidiplomasia kukamilika.

Kwa upande wa Makamishna wa Polisi, Balozi Sefue amewataja walioteuliwa kuwa ni:

1. Naibu Kamishna wa Polisi **Simon Nyakoro Sirro** ambaye amepandishwa cheo kuwa Kamishna wa Polisi, na ameteuliwa kuwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam. **Kamishna Sirro** anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Kamishna Mstaafu Suleiman Kova.
2. Naibu Kamishna wa Polisi **Albert Nyamuhang'a** ambaye amepandishwa cheo kuwa Kamishna wa Polisi na ameteuliwa kuongoza Idara ya Fedha, Utawala na Lojistiki. **Kamishna Nyamuhang'a** anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Kamishna wa Polisi Clodwing Mathew Mtweve aliyeoteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza.
3. Naibu Kamishna wa Polisi **Robert Boaz Mikomangwa** ambaye amepandishwa cheo kuwa Kamishna wa Polisi na ameteuliwa kuongoza Idara ya Intelijensia. **Kamishna Mikomangwa** anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Kamishna Valentino Mlowola aliyeoteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

4. Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi **Nsato Marijani MSSANZYA** ambaye amepandishwa cheo kuwa Kamishna wa Polisi na ameteuliwa kuongoza Idara ya Mafunzo na Operesheni. **Kamishna MSSANZYA** anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Kamishna wa Polisi Paul Moses Chagonja aliyeuleliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi.

Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli amemteua **Dkt. Modestus Francis Kipilimba** kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Kabla ya Uteuzi huu Dkt. Kipilimba alikuwa Mkurugenzi wa Menejimenti ya Udhibiti (*Director of Risk Management*) katika Benki Kuu ya Tanzania. **Dkt. Kipilimba** anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Dickson Maimu ambaye uteuzi wake ultenguliwa.

Teuzi zote zinaanza leo tarehe **15 Februari, 2016**.

Gerson Msigwa

Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano, IKULU

Dar es salaam

15 Februari, 2016